

**HOTUBA YA MGENI RASMI MHESHIMIWA MHE. DKT.
ASHATU KACHWAMBA KIJAJI (MB) NAIBU WAZIRI WA
FEDHA NA MIPANGO, KWENYE MAHAFALI YA 39 YA BODI
YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU (NBAA)
TAREHE 30 SEPTEMBA 2017**

Mwenyekiti wa Bodi ya NBAA, CPA. Prof. Isaya J. Jairo
Waheshimiwa Viongozi wa Vyama na Serikali;
Wakurugenzi wa Bodi ya NBAA;
Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA, CPA Pius Maneno,
Wahisani wanaotoa zawadi kwa Watahiniwa bora,
Wafanyakazi wa NBAA;
Ndugu Wahitimu;
Wageni Waalikwa;
Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote kwa kutuweka salama hatimaye tukaweza kukutana siku hii ya leo ya mahafali ya 39 ya kuwatunuku wahitimu wa uhasibu katika Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA). Nichukue pia fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Bodi pamoja na uongozi mzima wa NBAA kwa kunialika kwa mara nyingine kuwa Mgeni Rasmi katika sherehe ya mahafali ya NBAA. Ni furaha kubwa sana kwangu kuona umati mkubwa wa wageni waliofika hapa kushiriki tukio hili muhimu la kushuhudia ndugu na jamaa zao wakitunukiwa vyeti vyao. Nachukua nafasi hii kuwapongeza wahitimu wote

mnaohitimu leo hii katika ngazi ya taaluma ya juu ya uhasibu (CPA), mnaohitimu katika ngazi ya cheti cha uhasibu na wale mnaohitimu katika ngazi ya Sta-shahada ya viwango vya hesabu za taasisi za umma (Diploma in IPSAS). Mafanikio mliyoyapata yanatokana na jitihada zenu zilizowawezesha kufaulu mitihami yenu. Hongereni sana!

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa,

Kuhitimu katika fani yoyote ile ni matokeo ya jitihada za muda mrefu si kwa wahitimu wenyewe tu bali pia hata kwa wale waliowasadid kufikia hatua hii. Wapo walimu waliowafundisha, wapo wazazi/walezi waliowalipia ada za masomo, wapo waliolipiwa ada na serikali au na waajiri wao na wengineo wengi ambao siwezi kuwataja wote hapa. Kwa ujumla nawashukuru na kuwapongeza wote.

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa,

Nachukua nafasi hii kuipongeza Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) kwa kazi kubwa ya kuwaandaa watahitimu hawa hadi kufikia hatua hii. Nafahamu na napenda kusema mbele ya Wageni waliopo hapa kwamba NBAA ni kati ya taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ambayo imekuwa ikitoa msaada na mchango mkubwa sana katika kufanikisha shughuli za Wizara. NBAA imekuwa ikitoa michango mbalilmbali hasa ile ya kitaalamu katika shughuli za usimamizi wa fedha, uandikaji wa taarifa za fedha katika viwango vya kimataifa pamoja na kuchangia katika kuandaa

bajeti ya serikali inayosomwa Bungeni kila mwaka. Kwa kweli nachukua fursa hii kuipongeza zana Bodi hii na hasa ukizingatia kuwa iko chini ya Wizara ya Fedha ambayo ninaiongoza.

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa,

Napenda kuwapongeza sana NBAA kwa kuendesha shughuli mbalimbali za kuendeleza taaluma hii ya uhasibu kwa weledi wa hali ya juu. Pia nawapongeza NBAA kwa kuwa wabunifu katika kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazoikabili taasisi. Mfano mzuri ni ujenzi wa Kituo hiki cha Uhasibu hapa Bunju. Huu ulikuwa ni ubunifu wa Bodi na Menejimenti ya NBAA katika kuhakikisha kuwa taasisi inaboresha ufanisi wa kazi zake, inaongeza mapato yake na wakati huo huo inabana matumizi. Nawapongeza sana kukamilisha ujenzi wa kituo hiki katika ubora wa kuvutia na kuridhisha.

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa,

Uchumi wa mataifa yote duniani unategemea sana wataalamu wa fedha na uchumi. Mataifa yaliyoendelea kiuchumi yalijikita zaidi katika kuwafundisha vijana wao utaalamu mbalimbali na hatimaye kila sekta ikawa na wataalamu wenye fani inayohusika na sekta hiyo. Sekta ya uchumi na fedha ni kati ya sekta ambazo hupewa kipaumbele kikubwa kutokana na umuhimu wake. Tunafarijika sana tunapoona wataalamu hawa wa fedha wakiongezeka hapa nchini kwetu mwaka hadi mwaka. Kama alivyosema Mwenyekiti kuwa mwaka huu ni moja kati ya miaka

ambayo idadi ya wataalamu hawa imeongezeka kwa kiasi kikubwa. Nawapongeza sana NBAA kwa kutambua kuwa ongezeko hili la wahasibu na wakaguzi wa hesabu litakuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha uchumi wa viwanda ambao Serikali yetu ya awamu ya tano inataka kuujenga. Nafahamu fika kuwa ujenzi na uendeshaji wa uchumi wa viwanda unahitaji usimamizi ulio bora wa fedha na watakaoliwezesha hilo ni pamoja na nyie wataalamu mnaohitimu leo.

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa,

Nafahamu kuwa NBAA inajitahidi sana kutekeleza jukumu la kuhakikisha kuwa wataalamu wa masuala ya fedha wanaongezeka hapa nchini na hivyo inastahili kupongezwa.

Hata hivyo NBAA bado inatakiwa kuongeza bidii katika kuhakikisha kuwa idadi ya wataalamu hawa inaendelea kuongezeka kwani bado mahitaji yao hayajafikiwa. Kwa takwimu tulizonazo, idadi ya wahasibu wote wenye sifa hawatosherezi hata mahitaji ya sekta ya umma pekee achilia mbali sekta binafsi. Hivyo kuna umuhimu kwa NBAA kuendelea kuhakikisha kuwa ufaulu wa watahiniwa wake unaendelea kuongezeka.

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa,

Pamoja na kutaka kuongezwa kwa idadi ya wataalamu wa uhasibu na ukaguzi hesabu, msisitizo mkubwa lazima uwekwe kwenye kuzalisha wataalamu wenye weledi wa hali ya juu. Pia ni jukumu la NBAA

kuendelea kusisitiza mara kwa mara kwa wanachama wake umuhimu wa kuzingatia misingi ya uaminifu na uadilifu katika kazi zao za kila siku. Nina uhakika wataalamu hawa wa masuala ya fedha wakitimiza wajibu wao kikamilifu uchumi wa Taifa letu utaendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha. Maana matatizo ya ufisadi na ubadhilifu katika Serikali na Taasisi zake yatapungua kwa kiasi kikubwa kama sio kumalizika kabisa.

Nina hakika kuwa wahitimu hawa wameiva kitaaluma na wako tayari kulitumikia Taifa kwa nguvu zao zote, kwa weledi wa hali ya juu na kwa kufuata misingi ya uaminifu na uadilifu. Wako wale ambao tayari wako makazini na waliamua kujiendeleza. Naamini wataenda kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi baada ya kuhitimu masomo haya ya uhasibu. Wale ambao wamehitimu na bado walikuwa hawajaajiriwa ni matumaini yangu makubwa kuwa maarifa na ujuzi walioupara katika masomo yao utawarahisishia kupata kazi nzuri na kwa urahisi zaidi. Bado soko la ajira katika fani ya uhasibu ni kubwa na naamini kuwa wataajiriwa hivi karibuni.

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa;

Pamoja na kwamba soko la ajira katika fani ya uhasibu hapa nchini bado ni kubwa, ipo haja kwa wahitimu wa fani hii kutumia utaalamu walioupara ili kujitafutia ajira binafsi mfano kufungua miradi mbalimbali ya kibiashara. Mhasibu anajua jinsi ya kuweka hesabu vizuri na hivyo hata akikopa fedha benki kwa ajili ya biashara ni rahisi kusimamia mkopo huo ili kufanikisha biashara yake na hatimaye kurudisha mkopo kwa wakati. Hii ni tofauti na wale watu waliosoma fani nyingine zisizo

za kihasibu. Tunategemea wahitimu wa fani ya uhasibu wazalishe ajira hapa ili kuisaidia Serikali kukabiliana na upungufu wa ajira hapa nchini.

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa,

Kama tunavyofahamu kuwa katika nchi zetu za Afrika Mashariki kumekuwa na ugunduzi wa rasilimali ya mafuta na gesi. Rasilimali hizi zinahitaji kusimamiwa na kuendelezwa vizuri ili kuleta tija inayotarajiwa katika maendeleo ya uchumi wa nchi zetu. Kada ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu chini ya NBAA inatakiwa kujipanga sawasawa katika kusimamia uandishi na ukaguzi wa hesabu zinazohusu masuala ya mafuta na gesi ili kuleta maendeleo yanayokusudiwa.

Kama ilivyo kwa masuala ya madini, masuala ya mafuta na gesi ni nyeti na yanahitaji uangalizi na usimamizi wa hali ya juu. NBAA inatakiwa kujipanga kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na wataalamu wa kutosha na wenyewe ujuzi na weledi unaohitajika katika nyanja ya uhasibu na ukaguzi hesabu za masuala ya mafuta, gesi na madini kwa ujumla, ili kufanikisha nia na lengo kubwa la Serikali la kuhakikisha kuwa rasilimali za nchi zinatumika kwa manufaa ya Watanzania wote.

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa,

Ili kufanikisha hayo yote NBAA inatakiwa kuboresha utendaji wake wa kazi na kuacha kufanya kazi kwa mazoea. NBAA inatakiwa kuboresha utoaji huduma kwa wateja wake kama vile wanafunzi, wanachama na

wananchi wote kwa ujumla ili kuendana na kasi ya Serikali ya awamu ya tano. Ushindani unaotokana na utandawazi unawalazimisha kuboresha huduma zenu kwa wateja na utendaji wenu wa kazi. Kinyume cha hayo mjue kuwa mtapoteza wateja wenu na kushusha mapato yenu.

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa,

NBAA ikiwa ni taasisi ya Serikali, kwa muda mrefu imekuwa ikiishauri Serikali katika masuala ya uhasibu, ukaguzi wa hesabu, usimamizi wa fedha na juu ya vyanzo vya mapato ya Serikali. Naiomba NBAA iendelee na kazi hii nzuri ya kuishauri Serikali katika mambo hayo ya kitaalamu ili kuongeza tija ya utendaji wa Serikali katika nyanja hizo. Naahidi kwa niaba ya Serikali kuwa tutaendelea kuuthamini ushauri wote wa kitaalamu kutoka NBAA na kuufanya kazi kadri itakavyooneka inafaa.

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa,

Kama tunavyofahamu nchi yetu ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuwa katika Jumuiya kuna fursa na changamoto nyingi zinazotokana na kuungana. Nauomba uongozi wa NBAA kuwa wabunifu na kuzitumia fursa zinazopatikana kwa Tanzania kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini pia iwe tayari kuzikabili na kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazoweza kujitokeza. Changamoto hizo ni pamoja na soko la bidhaa au huduma zinazotolewa na NBAA pamoja na wanachama wake. Wahasibu na Wakaguzi wa

Hesabu hapa nchini wanatakiwa wawe mstari wa mbele kuhakikisha kwamba Tanzania inangára katika soko la Afrika Mashariki na nje. Tunataka wataalamu wetu watoke na kwenda kutoa huduma katika nchi nyingine. Na huduma zitakazotolewa ziwe katika viwango vya hali ya juu.

Ili kuzikabili changamoto na kuzitumia vizuri fursa zinazotokana na Tanzania kuwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, NBAA inatakiwa kuhakikisha kuwa inatoa wataalamu wenyewe ujuzi na weledi wa viwango vya kimataifa ambao watakubalika katika nchi zote za Afrika Mashariki, Afrika na Duniani kwa ujumla. Pia NBAA inatakiwa kuhakikisha kuwa wataalamu hawa wanaendelea kujiendeleza na kuimarishe ufahamu wao katika masuala mbalimbali ya uhasibu na ukaguzi hesabu kupitia mafunzo na semina mbalimbali zinazoandaliwa na NBAA.

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa;

Kwa upande wa Serikali, tunaahidi kuendelea kushirikiana na NBAA katika kutatua changamoto mbalimbali za kiutawala ikiwemo kuhakikisha NBAA inakuwa na wafanyakazi wenyewe ujuzi na weledi wa kutosha ili kutekeleza majukumu yake. Serikali itahakikisha kuwa NBAA inaendelea kuwa na wafanyakazi wenyewe utaalamu na ujuzi unaostahiki katika kutimiza majukumu ya Bodi kwa weledi.

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa;

Ili kuboresha taaluma ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu hapa nchini NBAA inatakiwa kuendelea kushirikiana na Bodi nyingine za nje kwa ukaribu zaidi. Ni vizuri sana kujifunza kwa wengine. Kila siku kuna kitu kipyta cha kujifunza na unaposhirikiana na mwenzako ndipo unafahamu zaidi. Nimefurahi kusikia kuwa tayari NBAA imesaini mkataba wa ushirikiano ‘Memorandum of Understanding’ na Bodi nyingine za uhasibu katika nchi za Afrika ya Mashariki. Hii ni hatua nzuri sana. Jitihada zaidi zifanyike na NBAA ili kusaini mikataba mingi zaidi ya ushirikiano na Bodi nyingine duniani ili kujifunza mengi zaidi na kuifanya taaluma ya uhasibu hapa nchini itambulike zaidi ndani na nje ya nchi.

Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa;

Nirudie tena kuwapongeza sana nyie wote ambao leo mnatunukiwa vyeti na baadhi yenu kupewa zawadi mbalimbali kwa kufanya vizuri zaidi katika masomo yenu. Nafahamu kwamba kuna wengine wengi ambao nao walitamani sana kutunukiwa vyeti leo hii lakini bado hawajafanikiwa. Nawaomba wasikate tamaa hata kidogo bali waendelee kujitahidi hadi nao waweze kufikia hatua hii.

Ndugu Wahitimu, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Naomba nimalizie kwa kutoa tena shukrani zangu za dhati kwa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu kwa kunialika katika

mahafali haya. Nimefurahi sana kuwa pamoja nanyi katika mahafali haya ya 39. Nawatakieni wahitimu wetu kila la kheri katika maisha yenu.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.